**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 05 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

**I. WIMBO WA TAIFA.**

**II. DUA.**

**III. KIAPO CHA MJUMBE:**

Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad

**IV. TAARIFA YA SPIKA:**

**V. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 26 Februari, 2021.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka 2021/2022.

## VI. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

22. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Wakaazi wengi wa vijijini ni wenye kipato cha chini, ambao hushindwa kumudu gharama za ujenzi wa nyumba za kisasa. Hata hivyo, kwa upande wa Jeshi la Polisi la Tanzania, wakati walipojenga nyumba za kuishi kwa wanajeshi katika eneo la Mfikiwa Chake Chake Pemba, walitumia matofali yenye gharama nafuu na yasiyohitaji saruji nyingi katika ujenzi

    Je, ni lini Serikali kupitia Jeshi la Polisi itaandaa utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wananchi, kuhusu utengenezaji wa matofali ya bei nafuu ili watu wenye kipato cha chini waweze kupata makaazi bora na ya kudumu.

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

100. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

    Kwa muda mrefu sasa wananchi wa Tomondo wamekuwa na kilio kutokana na athari ya kujaa ziwa maboga katika kila kipindi cha msimu wa mvua. Suala hili limeshakuwa la muda mrefu na ahadi

ya Serikali imekuwa ya muda mrefu kupata ufumbuzi wa kudumu wa athari hiyo.

(a) Je, kuna mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Tomondo kuondokana na athari ya kujaa kwa ziwa maboga.

(b) Je, Serikali imewahi kutoa ahadi ya kufanya utafiti wa athari za kimazingira katika eneo la ziwa maboga, na je, utafiti huo umefanyika na matokeo yake ni yepi na kama bado lini utafanyika.

(c) Je, wananchi wa Tomondo wategemee lini kilio chao kitapatiwa ufumbuzi wa kudumu na Serikali.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

68. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa,Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mwanzoni mwa mwaka 2020, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Halmashauri ya Jiji la Zanzibar. Hata hivyo, wananchi wengi bado hawajaelewa majukumu, mamlaka na utawala pamoja na mali zinazomilikiwa na Jiji hilo.

(a) Je, ni shughuli gani zinazofanywa na jiji la Zanzibar pamoja na mali zinazomilikiwa kwa mujibu wa Sheria.

(b) Zipo habari kwamba viongozi wanatumia mali za Manispaa ikiwemo magari, Je taarifa hizi ni za kweli na kama ni kweli Serikali imejipanga vipi kuwapatia usafiri viongozi hao ili wasitumie magari ya Manispaa.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia na Watoto:</u>**

149. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MANDOBA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Naipongeza Serikali kwa kuweka mashine katika sehemu zote zinazopita wasafiri kama bandarini na Uwanja wa ndege, Mashine hizo ni kwa ajili ya kuwapima joto la mwili na kuona dalili za awali kutokana na maradhi ya kupumuwa.

Je, ni kwa nini mashine hizo hazitumiki kwa lengo lililokusudiwa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

125. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mwaka huu Serikali kwa kupitia NACTE imezuiya udahili wa wanafunzi waliofanya mitihani ya kidato cha nne mwaka 2020 kujiunga na vyuo pasi na kuzingatia matokeo ya wanafunzi husika.

(a) Je, hatuoni kama tumewanyima wanafunzi haki yao ya kujiendeleza kielimu.

(b) Je, hatudhani kuwa maamuzi haya yanaweza kusababisha madhara kwa baadhi ya wanafunzi wa kidato cha nne.

(c) Je, ni sababu zipi zilizopelekea wanafunzi hata ambao hawana sifa za kujiunga na kidato cha tano na sita kuzuiwa kujiunga na vyuo vikuu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

58. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumejitokeza tatizo kwa baadhi ya wafanyakazi waliostaafishwa mwaka 2018/2019 katika Shirika la Bandari kukatwa fedha zao kwa asilimia 40%.

(a) Je, ni wafanyakazi wangapi waliostaafishwa mwaka 2018/2019.

(b) Je, ni sababu gani iliyopelekea kukatwa fedha hizo.

**VII. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**5 Mei, 2021.** **KATIBU WA BARAZA.**